

Publication: MTANZANIA

Country: Tanzania

Date: 27/05/2011

# Dk. Bilal aeleza njia za ajira kwa vijana

**Na Rachel Mrisho,****Dar es Salaam**

MAKAMU wa Rais, Dk. Mohammed Gharib Bilal, amesema nchi za Afrika zinaweza kukabiliana na tatizo la ajira za vijana endapo zitakuza sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT).

Akizungumza juzi jijini Dar es Salaam wakati wa ufunguzi wa mkutano wa sita wa Elimu Mtandao (eLearning Africa), Dk. Bilal alisema; "Hivi sasa nashuhudia ongezeko kubwa katika uwekezaji katika ICT"

"Afrika ina idadi kubwa ya vijana wanaokua haraka, lakini fursa mpya za ajira haziendani na kasi hiyo ya ukuaji, vijana barani Afrika ni asilimia 37 ya umri ambao unaruhusu wawepo kazini lakini asilimia 60 kati yao hawana ajira.

"Fursa za ajira hazijaendana na ukuaji wa idadi ya vijana ambao wako tayari kuajiriwa kwa sababu shughuli za uchumi hazijaongezeka kiasi cha kuweza kuwa na uwezo wa kutosha kutoa ajira toshelevu, vijana wengi hawana ujuzi, utaalamu na uzoefu unaotakiwa katika soko la ajira," alisema Dk. Bilal

Kutokana na hali hiyo, vijana wanahitaji utaalamu na ujuzi utakaowafanya waendane na ushindani wa soko la ajira na hivyo kuwawia rahisi kuajiriwa na kuzalisha mali kitaalamu.

Dk. Bilal alisema kwamba, kasi ya ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na shule au vyo imetoa changamoto kadhaa ikiwamo upungufu wa walimu wenye sifa za kutosha, ukomo wa upatikanaji wa maabara na intaneti, vifaa vya kufundishia na maabara.

Alishauri ili kukabiliana na changamoto hizo za elimu, ni vyema kwa serikali kuwekeza teknohama shuleni na vyooni na programu zinazohusiana na ICT.